# KYELA COOPERATIVE UNION LIMITED

## REG:AFF-MBY-KYC-DC-2022-2

**TANGAZO LA ZABUNI YA USAMBAZAJI WA MAGUNIA AINA YA JUTE YATAKAYOTUMIKA KUTUNZIA KAKAO ZINAZOKUSANYWA NA VYAMA VYA MSINGI VILIVYOPO KATIKA WILAYA YA KYELA.**

**ZABUNI NAMBA:** KYC/2025/2026/G/01

**MWAKA WA FEDHA:** 2025/2026

**TAREHE YA TANGAZO:** 16 OCTOBER, 2025

**TANGAZO LA ZABUNI**

Chama Kikuu cha Ushirika cha Kyela (KYECU LTD) kilichosajiliwa chini ya sheria ya vyama vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013, kinawatangazia Wazabuni na wananchi wote wa Tanzania kuwa KYECU LTD inahitaji Msambazaji mwenye uwezo na Uzoefu wa kusambaza magunia mapya, Tupu ya kuhifadhia kakao kwa mwaka 2025/2026, Sawa na kibali cha Mrajis chenye **Kumbu Na. LA.69/209/05/69.**

| NAMBA YA ZABUNI | AINA YA ZABUNI |
|---|---|
| **KYC/2025/2026/G/01** | **ZABUNI YA USAMBAZAJI WA MAGUNIA AINA YA JUTE YATAKAYOTUMIKA KUTUNZIA KAKAO ZINAZOKUSANYWA NA VYAMA VYA MSINGI VILIVYOPO KATIKA WILAYA YA KYELA.** |

**A. MAELEZO/SIFA YA ZABUNI/BIDHAA INAYOTAKIWA KUSAMBAZWA.**

1.Msambazaji awe na uwezo wa kusambaza gunia zenye sifa zifuatazo:

- Gunia lenye uwezo wa kubeba KG 70 za kakao;
- Gunia zilizotengenezwa kwa JUTE;
- Kipimo chake ni (44*26.5) inch;
- Uzito wa gunia ni 2.25lbs (1020gms);
- Gunia liwe na uwezo wa kushona kichwa/sandarusi kwa haraka;
- Gunia lenye rangi asilia yenye mistari miwili ya blue, laini/lenye alama;
- Gunia lenye Nembo ya food grade;
- Kiasi cha Gunia kinachohitajika kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni gunia 135,000 tu sawa na belo 450 zilizofungashwa gunia mia tatu (300);
- Msambazaji anatakiwa kusambaza gunia mara baada ya mkataba kusainiwa;
- Msambazaji anatakiwa kufikisha Gunia hadi ghala kuu la KYECU LTD;

**MASHARTI YA MWOMBAJI.**

1. Mwombaji lazima awe Mtanzania;
2. Mwombaji awe na kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania (Ambatanisha cheti cha usajili wa kampuni);

3. Mwombaji awe na hati hai ya kuthibitisha ulipaji kodi (TAX CLEARANCE CERTIFICATE);
4. Mwombaji lazima awe na leseni ya biashara husika iliyo hai;
5. Mwombaji lazima aambatanishe namba ya utambulisho ya mlipa kodi (TIN);
6. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha na athibitishe kwa kuambatanisha taarifa za benki (**Bank statement**) ya Miezi kumi na mbili (12), iliyopita kutoka tarehe aliyoomba zabuni na lazima iwe imethibitishwa na BANK husika na kugonga muhuri na iwe original inayosomeka vizuri;
7. Mwombaji awe na Taarifa za fedha zilizokaguliwa (Audited financial statement) kwa kipindi cha miaka miwili (2) Mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2023/2024;
8. Mwombaji ambatanishe 'Power of Attorney' inayosimama na kuongelea zabuni husika;
9. Ada ya maombi ya zabuni ni Tsh.1,000,000/= (Millioni moja tu),
   Kiasi hicho kitalipwa kupitia akaunti ya chama **No. 261208000001** jina la akaunti Kyela Cooperative Union Ltd (Benki ya TCB) na kukatiwa stakabadhi ya malipo ambayo itaambatanishwa katika barua ya maombi ya zabuni na fedha hizo hazitarudishwa;
10. Mwombaji asiwe amehusika na migogoro yoyote na vyama vya Ushirika Tanzania;
11. Mwombaji asiwe amewahi kusababisha hasara yoyote katika shughuli ya Usambaji wa gunia;
12. Mwombaji awe na uzoefu wa kufanya kazi za usambazaji wa gunia kwa muda usiopungua miaka miwili (2) na aambatishe nakala ya uzoefu kama vile mikataba pamoja na tuzo ya kukubaliwa kufanya kazi;
13. Zabuni zitashughulikiwa kwa utaratibu wa ushindani wa kitaifa (National competitive Tendering) kama uliyoainishwa kwenye Mwongozo na Sera ya Ununuzi na Ugavi wa Vyama vya Ushirika.
14. **Masharti ya nyongeza kwa mwombaji:-**
    i. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha kwa ajili ya kulipa wafanyakazi wake kwa wakati;
    ii. Mwombaji aweke kiasi atakacholipa/atakacholipwa kwa kazi aliyoomba;
    iii. Mwombaji atahifadhi magunia katika maghala ya KYECU LTD na atatumia ofisi zilizo katika eneo la KYECU LTD TU.
    iv. Muombaji awe na risiti ya EFD kwa ajili ya kutoa risiti ya kukiri mapokezi ya Fedha;
    v. Mwombaji aambatanishe taarifa binafsi za kampuni na uthibitisho wa kampuni kwa nyaraka zilizothibitishwa na mwanasheria.

15. Kitabu cha zabuni na maelezo mengine vitapatikana katika ofisi ya Meneja Mkuu **KYECU LTD, S.L.P 415, KYELA** Kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 9.30 alasiri (Jumatatu hadi Ijumaa) na siku ya jumamosi ni saa 2.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana isipokuwa siku za sikukuu.
16. Maombi yazingatie mahitaji na kuambatanisha viambatanishi kama vilivyoainishwa katika Tangazo la Zabuni na Kitabu cha Zabuni na kutumwa kwa **MENEJA MKUU KYECU LTD, S.L.P 415, KYELA.**
17. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (Original) moja(1) na nakala (Copy) moja (1) zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri.
18. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya **E-MAIL, FAX,TELEFAX na TELEGRAFIC SYSTEM** hayatapokelewa na kufunguliwa siku ya ufunguzi.
19. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **23/10/2025 saa 4:00** asubuhi na kufunguliwa tarehe **23/10/2025** saa **4:30** asubuhi katika ofisi za **KYECU LTD.** Waombaji mnakaribishwa katika ufunguzi wa zabuni kwa gharama zenu.
20. Zabuni ifungwe kwa rakili na iandikwe juu ya bahasha namba ya zabuni unayoomba.
21. Zabuni itakayochelewa kuwasilishwa, na isiyofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni kwa hali yoyote haitakubaliwa kwenye Tathimini.
22. Maombi yote yawekwe kwenye sanduku la zabuni lililopo katika ofisi ya Chama kikuu cha Ushirika Kyela (KYECU LTD).

-----------------------------

**LEAH MWAKAPALA**
**MWENYEKITI WA BODI**
**KYECU LTD.**

KYECU LIMITED
16 OCT 2025
PO BOX 415, KYELA
MBEYA